

Jeshi kupewa dhamana ya kuulinda msitu wa Derema

Na Jacqueline Tesha - Mratibu Kanda ya Kaskazini

Msitu wa Derema Corridor ambao upo katika tarafa ya Amani, wilayani Muheza mkoani Tanga, umekua ukikumbwa sana na matukio mengi ya uharibifu, likiwemo lile la uvunaji wa miti kiholela pamoja na uchimbaji madini katika vyanzo vya maji. Tatizo hili la uvunaji wa miti limekua sugu sana hasa katika maeneo ya vijiji vya Kwezitu, Kambai na Kwatango.

Hii imepelekea wananchi wanaozunguka maeneo ya msitu wa Derema kukerwa kwa kuongezeka kwa vitendo hivyo huku kukiwa hakuna hatua madhubuti zozote zinazochukuliwa kukomesha hali hiyo. Wananchi hawa waliamua kumpigia simu Mkuu wa Wilaya ya Muheza Mh. Mathew Nassai na kumweleza juu ya uharibifu huo uliokua ukiendelea katika maeneo hayo ya msitu. Mkuu huyo wa wilaya alichukua hatua ya kwenda katika eneo la tukio na kufanikiwa kukamata mbao zaidi ya 1,200 ambazo zilikuwa zimefichwa katika maeneo ya msitu huo karibu na kijiji cha Misalai ambazo zinasemekana kuwa ni mali

ya kampuni moja ya chai wilayani huko. Katika tukio jingine lilionekana lori likitoka katika maeneo ya msitu huo likiwa limesheheni mbao, jitihada za kulifuatilia na kulikamata zilifanywa lakini hazikuzaa matunda. Na hii ilisababisha kubadilishwa kwa walinzi wa geti la kutokea Amani Nature Reserve ili kuweza kuimarisha ulinzi na kupunguza kufahamiana. Mabadiliko haya yalionekana kutozaa matunda maana baada ya siku chache mbao takribani 129 zilikamatwa katika kijiji cha Kwezitu na wanamtandao wa MMIKAZI, na baadae zikakamatwa

tena mbao 120 katika kijiji hicho hicho na mwishoni kufanikiwa kukuta lundo la mbao ambazo zilikuwa zimehifadhiwa katika banda la mbuzi katika kijiji hicho cha Kwezitu. Mbao zote zilikamatwa na kuhifadhiwa Amani Nature Reserve, isipokua hizo za kwenye banda la mbuzi maana zilisemekana zilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa soko la kijiji, taarifa ambayo ilitolewa kwa Mwenyekiti wa Kijiji hicho cha Kwezitu.

Mh. Mathew Nassai aliamua kurudi tena katika maeneo hayo na timu yake na kuamua kutembelea maeneo yenye uharibifu mkubwa na kisha kufanya

mikutano na Serikali za kijiji na baadae kuitisha mikutano ya hadhara kwa kila kijiji, hii ilifanyika katika vijiji vya Kambai, Kwatango, Magoroto, Kwezitu na Mlesa. Vikao vyote hivi vilikua vikijadili kuhusiana na tatizo la uvunaji miti pamoja na uchimbaji wa madini, na kutafuta suluhu ya matatizo hayo. Pia Mkuu huyo wa wilaya aliwasiliana na Mkuu wa wilaya ya Mkinga ili naye aweze kuitisha vikao na

mikutano kama yake katika vijiji ambavyo vinapakana na wilaya ya Muheza.

Jitihada za kumtafuta Mkuu wa Wilaya ya Muheza zilifanikiwa na haya ndiyo yalikuwa maneno yake "Ni kweli nimekua nikipokea taarifa nyingi toka kwa vijana wa mitandao yenu kuhusiana na uchimbaji wa madini pamoja na uvunaji wa msitu, na nilijitahidi kutoa ushirikiano wa haraka kila nilipopewa taarifa, lakini baada ya kuona uhalifu bado unazidi kuendelea



Kiongozi wa Serikali ya kijiji akielezea kwa waandishi kuhusu uharibifu unaondelea katika

ndipo nilipoamua kwenda mwenyewe kushuhudia kwa macho yangu na kisha kuitisha mikutano ya vijiji ili tuweze kujadiliana na viongozi wa serikali za vijiji na wanajamii wote juu ya njia za kudhibiti uharibifu huo uliokua ukiendelea, na ndipo wananchi walipokiri ya kuwa watajitahidi kila mmoja wao kuwa mlinzi wa msitu huo na kutoa taarifa za wahalifu pindi watakapowakamata. Kwa hiyo tumekubaliana hivyo na nategemea ushirikiano toka kwao, lakini kama watahindwa kutekeleza ahadi yao sitakuwa na njia nyingine zaidi ya kuwasiliana na Ofisi ya Mkoa wa Tanga na kuwapa kazi hiyo askari wetu (FFU au JKT) waliopo Kigombe kwa sababu kule tunalo jeshi zuri sana. Ili waje kutusaidia kufanya ulinzi katika maeneo hayo, ingawa nisingependa hali ifike hapo kwa sababu

najua madhara ya jeshi kushirikishwa katika swala kama hili.”

Pia Mkuu huyo wa Wilaya aliomba MJUMITA, TFCG pamoja na asasi nyingine ambazo zinahusika na uhifadhi wa misitu, kuragibisha juu ya udhibiti wa matumizi ya nyundo, na pia kuratibu mfumo ambao utakua ukipata taarifa toka katika viwanda vya mbao, ili kuweza kubaini ni aina gani ya mbao zinazolingia viwandani na zinazosafirishwa nchi za nje, na zinatoka katika msitu gani, na pia kiwekwe kiwango cha ubora wa mbao ambao utakua ukitumika kwa mbao zote zinazopelekwa viwandani na zile zinazosafirishwa nchi za nje. Anasema hii itasaidia kupunguza uvunaji wa kiholela katika misitu ya asili na hatimaye kurudisha hali za misitu hiyo kama ilivyokuwa hapo awali.